**64-0617  KRISTO ALIYETAMBULISHWA KATIKA NYAKATI ZOTE**

Jaribio La Msingi

Jina:____________________

Tarehe ya mwisho: Jumatatu, 30/Septemba/ 2024

**1. “Lakini nikizitenda, ijapokuwa hamniamini mimi, ziaminini zile________; mpate kujua na kufahamu ya kuwa Baba yu ndani yangu, nami ni ndani ya Baba.”**

[ ] Torati ya Musa

[ ] Mifano

[ ] Kazi

[ ] Wanafunzi

**2. Katika Biblia, Wayahudi walikuwa wakimwuliza Yesu maswali. Wayunani walimwuliza maswali. Na lilikuwa ni swali la sikuzote.**

[ ] Kwa sababu watu wengi sana wana fasiri nyingi sana za Yeye.

[ ] Kwa sababu kila mtu alitaka kuwa mwerevu

[ ] Kwa sababu kila mtu alitaka kumkaribia Mungu

[ ] Kwa sababu kila mtu alitaka kumjua Yeye zaidi

**3. Hakuna mtu aliyepata kusikia habari za Yesu pasipo wao kutamani kumwona.**

[ ] Kweli [ ] Uongo

**4. Ni neno gani ambalo maana yake ni, “nguvu zisizoonekana,” kama vile upepo?**

[ ] Elohimu

[ ] Shekina

[ ] En-morphe

[ ] Amoya

**5. “Yesu alisema ya kwamba, ‘Wale waliojiliwa na Neno, waliitwa’________,’” hao walikuwa ni manabii. Sasa, si kwamba mtu huyo mwenyewe alikuwa ni Mungu, si zaidi ya vile mwili wa Yesu Kristo ulivyokuwa ni Mungu. Yeye alikuwa ni mwanadamu, Naye Mungu alikuwa amefunikwa nyuma yake.”**

[ ] Masihi wadogo

[ ] Marabi

[ ] Miungu

[ ] Waonaji

**6. “Mungu daima ame______ kutoka kwa watu wote, na ku_______ Mwenyewe kwa watu watakaoamini hilo.”**

[ ] Jificha / Jifunua

[ ] Jionyesha / Jificha

[ ] Jifunua / Jificha

[ ] Chukuliwa / Jitoa

**7. “________ hulifunua kwa wasikilizaji, nao wasikilizaji wanaliamini. Ndipo, basi, huyo ni Mungu katika matendo, Mungu akitenda kazi kwa Roho Wake.”**

[ ] Mchungaji

[ ] Nabii

[ ] Mwalimu

[ ] Mwinjilisti

8**. “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo Mimi.”**

[ ] Kumbukumbu la Torati 18:15

[ ] Kutoka 19:4

[ ] Waebrania 4:12

[ ] 2 Nyakati 20:20

**9. “Mungu habadiliki. Tabia Yake haibadiliki. Yeye angali ni Neno, mnaona, na Malaki 3:6 inathibitisha hilo. Yeye hubadilisha tu umbo lake kwa kila________.”**

[ ] Wakati

[ ] Mtu

[ ] Kanisa

[ ] Kusanyiko

**10. Elohimu linamaanisha nini?**

[ ] “Nguvu isiyoonekana”

[ ] “Kitu cha kuabudiwa”

[ ] “Anayeishi peke yake”

[ ] “Yehova-Mwokozi”

**11. Ibrahimu alikuwa amemwona Mungu katika namna nyingi mbalimbali, alimwona Mungu katika njia gani kabla tu ya yule mwana aliyengojewa na kuahidiwa kutokea?**

[ ] Katika Nuru

[ ] Katika maono

[ ] Katika Mwanadamu

[ ] Kama hua

**12. “Bali wengi kadiri_________, Yeye huwarudi na kuwakemea.” Alisema kwamba ingekuwa jinsi hii katika wakati huu wa Kanisa la Laodikia.”**

[ ] Awapendao

[ ] Awachukiao

[ ] Awaitao

[ ] Awalaumio

**13. “Kumbukeni, Mungu hubadilisha umbo Lake.________, neno hilo la Kiyunani linamaanisha Yeye huvaa kinyago kingine.”**

[ ] Elohimu

[ ] Zoe

[ ] Amoya

[ ] En morphe

**14. Lakini Neno______ hulinyosha kosa.**

[ ] Daima [ ]Kamwe

**15. “Naye huwajia tu wale wanao_______. Kumbukeni hilo kote katika mkutano huu, Yeye atakutana tu na wale wanao_______!”**

[ ] Mtazamia

[ ] Mwomba

[ ] Simama upande Wake

[ ] Mngojea

**16. Kwa nini wale Wayunani walishindwa kumwona Yesu?**

[ ] Yeye alikuwa amevaa hekalu Lake la kibinadamu

[ ] Hawakuweza kufika mahali Yeye alipokuwa

[ ] Yeye daima aliondoka wakati wangalipo

[ ] Hakuna hata mojawapo juu

**17. “Malaki 4 na yote hayo yanapaswa kurudi moja kwa moja tena, Yeye tena kushuka na kujitambulisha Mwenyewe katika_________, kugeuza mioyo ya watoto irudi kwenye ile Imani; Imani ya mitume, ya pentekoste, ya wale baba zetu.”**

[ ] Kundi la watu

[ ] Kanisa

[ ] Baraza la Ekumeni

[ ] Ujumbe wa kinabii

**18. "Sasa, kumbukeni, mimi ni mtumishi Wake na wewe ni mtumishi Wake, Mungu ndani yangu na Mungu ndani yako. Una haja, nami nipo hapa kukutumikia, inaleta hayo pamoja na kuyafanya________."**

[ ] Halisi

[ ] Yatende kazi

[ ] Mmoja

[ ] Mungu

**19. Mungu anaishi wapi katika mwanadamu?**

[ ] Bongoni

[ ] Machoni

[ ] Moyoni

[ ] Yote hapo juu

**20. "Hili ndilo jambo la mwisho ambalo kanisa la Kikristo litaliona, katika ishara ya muujiza, mpaka kule kuonekana kwa Yesu Kristo. Kama Mungu amenipa kibali mbele yenu, niaminini katika Jina la Bwana, hakuna kitu kingine kilichosalia katika Biblia kutendeka ila_________; ninyi mna_______."**

[ ] Maangamizi / Ngome

[ ] Hukumu / Neema

[ ] Kuichukua alama ya mnyama / Muhuri wa Mungu

[ ] Moto wa milele / Uzima wa milele